# *Siku Hiyo Pale Kalvari*

Mungu akubariki Ndugu Neville na asante sana. Habari za asubuhi marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa Maskanini tena asubuhi ya leo kumtumikia Bwana kwa kulihubiri Neno na kuwaombea wagonjwa. Nami ninashukuru sana kwa ajili ya siku hii.

Nilishangaa mara tu nilipoingia. Ndugu alikuja akasema, "Sitaki kuwa kama yule mwenye ukoma asiyestahili aliyeponywa." Ilikuwa Ndugu Wright. Nilimwombea, naye Bwana amemponya kabisa. Ndipo akaja akilia kunipa mkono na kusema ya kwamba alitaka kumshukuru Bwana kwa kuponywa. Alitaka kurudi na kutoa shukurani. Wote umekwisha. Yeye ni mzima kabisa sasa. Tunashukuru kwa ajili ya shuhuda hizo.

Na lo, Charlie, wewe pamoja na Ndugu Jefferies, mkitaka kuja, njooni mketi kwenye viti hivi hapa, nanyi mnakaribishwa sana hivyo haitawabidi kusimama. Yule Ndugu mwingine pale, Ndugu Wood njoo hapa, kuna nafasi kadhaa hapa kwenye ubao wa kukalia, hivyo haitakubidi kusimama. Naamini kuna nafasi kadhaa hapa, naam, ndiyo, mmekaribishwa kabisa mje mketi mahali hapa.

Tunafurahi . . . Naamini ilisemwa wakati mmoja, "Nalifurahi waliponiambia, (Mungu akubariki Ndugu. Asante. Asante. Asante.) "Nalifurahi waliponiambia, 'Na twende nyumbani kwa Bwana.'" Hiyo ndiyo majaliwa ya Mkristo na furaha yake—kwenda katika nyumba ya Bwana.

Nikitazama kila mahali na kuwaona marafiki wangu wengi sana humu asubuhi ya leo, ninafurahi sana juu ya jambo hili. Nina furaha kumwona Ndugu na Dada Dauch hapa kutoka Ohio. Nawaona Ndugu na Dada Armstrong kule nyuma waliotoka Ohio. Mungu awabariki nyote pia. Na . . . Lo, ukitazama kila mahali unaona wengi sana, ingekuwa vigumu kutaja majina yao yote. Dada Hoover tunafurahi kukuona humu asubuhi ya leo kutoka kule Kentucky, na Charlie pamoja na Nellie, Ndugu Jefferies pamoja na jamaa yake na wengi sana humu kutoka nje ya mji huu.

Kwa hivyo tunatarajia wakati mzuri sana katika Bwana asubuhi ya leo. Tukimtarajia Mungu kukutana nasi kwa namna fulani apate kubariki nafsi zetu na kutuhudumia mambo tunayohitaji. Nami ninapoangalia kila mahali, kama nikianza kuwaita marafiki zangu walio humu, ningechukua karibu asubuhi mzima nikiwataja watu mbalimbali. Inanifanya nijisikie vizuri kurudi kanisani kuwaona watu wote humu na kukutana . . .

wanaoteseka ambao wamekuja wakiutafuta uponyaji. Nasi tutakutukuza kwa ajili ya jambo hilo. Tunaomba katika jina la Mwana Wako, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

Sasa katika mazungumzo ya asubuhi ya leo, tunataka kuwakumbusheni fungu la maneno niliyochagua kuzungumzia, *Siku Hiyo Pale Kalvari*. Inaonekana kama itakuwa nje kidogo ya wakati unaofaa. Hili linapaswa kuwa katika Ijumaa Kuu. Kalvari inapaswa kukumbukwa kila siku. Tumesikia mengi sana kuihusu. Tumesoma mengi sana juu yake. Wahubiri wameihubiri tangu mwanzo wa wakati. Waimbaji wameimba juu yake katika nyakati zote. Manabii walitabiri miaka elfu nne kabla haijatukia, na manabii wa siku hizi wanatuonyesha kule nyuma ilipotendeka. Ni siku muhimu sana.

Ni moja ya siku zilizo muhimu sana ambazo Mungu amepata kuzishusha duniani. Na kama ni muhimu sana kwa jamii ya kibinadamu, Kalvari, nafikiri ni vizuri kwetu kurudi nyuma tukachunguze tuone kwamba ina maana gani kwetu. Kwa kuwa nina hakika katika saa hii iliyochelewa tunayoishi, tunatafuta kila umuhimu wa Mungu tunaoweza kujua; na yote tunayoweza kujua, tuko hapa kujifunza hayo. Kuona ni yapi yaliyo yetu, na yale Mungu aliyotutendea, na kuona yale Yeye aliyoahidi kututendea. Na hilo ndilo linalotuleta kanisani.

Hiyo ndiyo sababu mhubiri huubiri. Hiyo ndiyo sababu yeye husoma na kuyatafakari Maandiko na kutafuta uvuvio—ni kwa sababu yeye ni mtumishi wa umma kwa watu wa Mungu, naye anajaribu kupata kitu ambacho . . . ambacho Mungu angewaambia watu Wake, kitu ambacho kingewasaidia. Labda huenda ikawa ni kuwahukumu katika dhambi zao, bali kingekuwa chenye manufaa kuwainua; wapate kuziacha dhambi zao kisha wainuke wakamtumikie Bwana. Nao wahudumu hawana budi kuyatafuta mambo haya.

Iwapo siku hii ni muhimu sana, moja ya siku zilizo kuu sana, hebu na tuangalie mambo matatu ambayo siku hiyo ilimaanisha kwetu. Tungechukua mamia. Bali asubuhi ya leo nimechagua tu mambo matatu tofauti yaliyo muhimu sana ambayo tunataka kuyachunguza katika muda mfupi ujao; ambayo Kalvari ilimaanisha kwetu. Nami naomba ya kwamba itamhukumu kila mwenye dhambi aliyeko, ya kwamba itamfanya kila mtakatifu kupiga magoti yake, ya kwamba itamfanya kila mgonjwa ainue imani yake kwa Mungu na aondoke ameponywa, kila mwenye dhambi aokolewe, kila aliyerudi nyuma arudi na ajionee aibu, na kila mtakatifu afurahi na apate tumaini jipya na tumaini jipya. Jambo moja kuu muhimu ambalo Kalvari inamaanisha kwetu na ulimwengu ni, ilimaliza swali la dhambi mara moja tu.

Mwanadamu alikuwa na hatia ya dhambi, na dhambi ilikuwa adhabu ambayo hamna mwanadamu aliyeweza kulipa. Adhabu ilikuwa kubwa sana hata hamna mtu angaliweza kulipa

